# *Njiani kuelekea kwenye utimilifu wa ufufuo*

*"Angalia, nawaambia ninyi siri; hatutalala sote,lakini sote tutabadilika, kwa dakika moja kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda Italia na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika. Maana sharti huu uharibikao uvae kutoharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa" (1Korintho 15:51-53)*

Sikiliza kile nabii wa Mungu alichosema juu ya hilo:

Angalia, katika njia yako kukuwa kuelekea kwenye utimilifu wa ufufuo, ukiongozwa na Roho.

Huwezi kuona kwamba tuko wakati wa mwisho? Yote yamekwisha kinachofuatia itakuwa ni uvumi wa haraka lile kundi dogo – pamoja katika mwezi mmoja au hivi litakuwa limekwenda, mara tu litakapokusanyika pamoja. Vema, tuko wakati wa mwisho hakuna matumaini popote. Enyi watu, kimbilieni kwa Kristo. (Matendo 1:1 – 11).

Na sasa, kumbuka, kama tunaenda kabla hajaja, tutakuwa juu na uweponi pake, au tutainuliwa kabla ya wengine hawajabadilishwa. Tarumbeta ya Bwana Italia, wafu walio katika Kristo watainuka kwanza. Halafu sisi tulio hai na tuliobakia tutabadilishwa kwa muda, katika kufumba na kufumbua na kunyakuliwa pamoja nao kumlaki Bwana hewani, "(1wathesalonike 4:13-17). Angalia ule utaratibu wa kunyakuliwa. Unaona, Mungu anajua tunahamu ya kuwaona wapendwa wetu., na kama tutaenda kumlaki Yeye kwanza, tutakuwa tunaangalia huku na huku kumuona kama ni mama au Baba na wengineo kama wapo. Lakini unaona, vile ambavyo Roho Mtakatifu ameliweka katika hekima yake? Tunakutana sisi wenyewe kwanza, na halafu tufikapo pale na kuimba "Neema ya Ajabu", hapa ndipo kutakuwa na muda wa kuabudu.

………………..mpaka hapo tarumbeta ya mwisho itakapopigwa. Na unajua tutanyakuliwa sote pamoja kumlaki Bwana hewani. Fikiria hilo. Watu watakosekana, hawakuoni wewe tena, lakini mnakusanyika wote pamoja na lile kundi lililotangulia. "wao waliohai watakao salia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hawatawatangulia (au hilo Neno ni kuwazuia) wao waliolala mauti. "sio waliokufa, hapana, wakristo hawafi. Wao wanachukuliwa tu



mapumzikoni kidogo; hilo tu. Oh, jamani. "Na tarumbeta ya Mungu Italia, na waliokufa katika Kristo, watafufuliwa kwanza na kuwatokea wengine…………….mara moja umetokea umesimama na kuangalia, na "vema, unamuona ni ndugu fulani…………."Najua sio muda mrefu. Katika dakika chache zijazo tutabadilishwa mara moja kufumba na kufumbua na kuwa pamoja nao tutakuwa tumetoweka duniani, tutanyakuliwa kumlaki Bwana hewani
(1 Korintho 15:15-15).

Na unaposema makaburi yatafunguka, ni kwa namna gani makaburi yataenda kufunguka wakati……………..sina muda wa kuliingilia hili, nilichohitaji ni kwenda kuchukua hili…………ili kukuonyesha urahisi wa Mungu. Na ile kalsiumpotash, (madini) na kila kitu wakati…………………… vitu vyote vilivyo ndani yako ni kijiko kimoja tuu……………………..Hiyo ni kweli. Na hiyo inafanya nini? Inapasuka na kuwa Roho ya uzima, ………………Mungu ananena tu unyakuo unakuja. Sio kwenda pale, na malaika washuke chini na machepe nje kule makaburini na kukuta mzoga wa zamani uliokufa hapa. Ni nini? Kwa kuanzia umezaliwa katika dhambi, lakini ule ni mpya uliotengenezwa katika kufanana Naye (1 Korintho 15:35-50).

Swali kwa ndugu Branham: Tutakuwa na sura gani katika kule kufufuka? Kama tulivyokuwa tulipokuwa tukizikwa. Hakika, kufufuka …………….Hebu waza hili kitabu hiki kinaanguka sakafuni, nami nikichukuwa kitabu hiki, kitabu tofauti nakukibadilisha. Huo sio ufufuo. Ufufuo ni "kuamsha yuleyule aliyezikwa" Je Yesu alifufuka? Je, walimjua? "Basi Yesu huyu aliyechukuliwa juu atarudi tena katika hali hiyo hiyo kama mlivyomwona Yeye akienda." Ufufuo ni kama tu unapokufa; hivyo ndivyo utakavyofufuka kama mwanadamu katika mwili. Na ndivyo ilivyo hasa. Kwa hiyo ufufuo ni vivyo hivyo. Tungechukua masaa mengi kwa hilo, lakini heri tusianze. Asubuhi ya pasaka alifufuliwa, na
(Matayo 27) inasema kwamba ikainuka miili mingi ya watakatifu walio lala katika mavumbi ya nchi; na waliingia katika mji na kuwatolea wengi. Matayo 27:5153. Jambo moja litakalofanyika ni kusubiri wakati wa mzunguko wa Mungu utimie mpaka wakati wa kuja mwana wa Mungu. Na kila kiumbe kilicho hai ambacho kilikufa ndani ya Kristo kitafufuka tena uweponi pake, kikimkumbatia Yeye. Oh nitakapofika mwisho wa safari yangu, Nataka nife katika uwepo Wake nilikuwa ninamkimbilia Yeye, kwamba ni ufufuo na uzima (Yohana 11:25-26). Yeye ni yule mmoja. Na Kanisa litakapofikia mahali hapo, mahali hapo, mahali ambapo Kristo ana maanisha sana kwetu kiasi kwamba tunaona kiu kuja uweponi pake na sisi kila mmoja na mwingine, hilo nichimbuko – liletalo – uzima. Hakuna shetani awezaye kukupita wewe. Hata kifo chenyewe kimeshindwa hapo. Oh ni tumaini la ajabu, ni mahali pa

namna gani! unafanywa upya mwenyewe. Na kwa kufanya hivyo unakumbuka kuwa Kristo ndiye ameyafanya haya yawezekane kwetu. Ni yeye aliyefanya mambo haya kwa ajili yetu. Lazima tumkumbuke yeye kwa maana ukumbuke kwanza tulitengwa tukawa maadui na Mungu, mataifa, tulichukuliwa na sanamu zisizo sema. Lakini kumbuka, Kristo siyo kwa wayahudi, bali kwa kila kiumbe wa uzao wa Adamu ulioanguka, Kristo alikufa (Waebra 2:8-10) Nilipokuwa nazungumzia usiku ule juu ya Ibrahim na uzao wake baada ya yeye; jinsi na namna ambayo Mungu alionyesha kupitia Ibrahim, Jinsi alivyo mhesabia haki Ibrahim, sura ya 12 ya mwanzo. Nakuendelea mpaka mwanzo 16, jinsi alivyolithibitisha lile agano kwa njia ya utakaso Mwanzo sura ya 17 alimuachia anyonye matiti yake kuchukua kutoka kwa
Roho Mtakatifu. Na halafu akalidhibitisha, na kumuweka mahali pake, akamchukua Ibrahim nje na kumbadilisha jina lake kutoka Abram kwenda Ibrahim; akampa sehemu ya jina lake., Elohim, h-a-m. Sasa tunaona kuwa baada ya hapo, Alimtokea Ibrahimu (Mwanzo 18).

Sasa, kwa uzao wake, angalia vile alivyoufanyia uzao wake jambo lilelile (Wagalatia 3:7-29). Uzao wa Ibrahimu umekuja kupitia kuhesabiwa haki, kutakaswa na ubatizo wa Roho Mtakatifu; udhihirisho wa jina lake, alijifunua kuwa yeye ni nani (Ufunuo ule wa ni nani? Yesu Kristo), ubatizo katika jina lake, kadhalika kama hivyo, ufunuo ule, akigawanya jina lake na kanisa lake, akawaita watoto. Halafu akafanya nini? Katika kanisa lile lile aliloliita kwa jina lake, Jina la Yesu, alifanya nini? Aliwatokea katika hali ileile alivyomtokea Ibrahim, akiwa na uwezo wa kupambanua roho nyuma yake. Alifanya hivyo? Alitokea katika Jina lilelile, kwa jambo lilelile, katika mfano uleule. Tuko tu mwisho wa safari /njia.

Sasa ona kile kilichofanyika. Alipofanya hivyo, hiyo ilikuwa ni ishara ya mwisho ambayo Alilipa kanisa kabla ya badiliko kuja katika kanisa, kwa Ibrahimu na Sara (Mwanzo 20). Sasa yule malaika alivyoeleza ile siri, yule mwanamke (aliwakilisha, kanisa) hakuliamini hilo kirahisi, alicheka moyoni mwake. Namalaika akasema “kwa nini yeye (mwanamke) amecheka? Kwa nini amefikiri hivyo? (mwanamke) moyoni mwake? Kwa nini alisema hivi? Sasa angalia. Hiyo ilikuwa ni ishara ya mwisho kabla ya jambo fulani kumtokea Sarah na Ibrahim (Mwanzo 18:9-15).

Sasa nilihubiri hapa wakati mmoja, na nilimwambia kuwa Mungu aliwabadilisha kuwa vijana mwanamume na mwanamke. Kulithibitisha hilo, aliendа kule chini, alikuwa na safari na kwenda Geradi, na Abimeleki, mfalme yule wa kifilisti, akampenda Sarah kimapenzi na akataka kumwoa. Na sasa unaona yeye alikuwa ni kijana msichana tena mrembo. Na angalia, alimfanyia



jambo fulani; Alimbadilisha yeye (Mwanamke). Hakuwafanya tu warudie ujana wao tu mwanaume na mwanamke, kijana mvulana na msichana; Hakufanya hivyo tu kwa sababu ingekuwa hivyo, jambo lilelile lingekuwepo unaona, wangekuwa …….”kwa sababu alimuoa akiwa msichana wa kama miaka kumi na sita, na alikuwa tu kijana mwanamume, na waliishi maisha yao yote bila mtoto. Kama angewarudisha tu kuwa vijana, vema, jambo lilelile lingekuwepo (utasa). Lakini ilibidi afanye jambo tofauti; ilibidi awabadilishe ili wampokee mtoto huyu wa ahadi walioahidiwa kumpokea. Lakini ilibidi abadilishe utaratibu wote wa maumbile, na kuwageuza tena kuwa vijana na kuwabadilisha wampokee mwana.

Jambo lilelile anaenda kulifanya tena, baada ya hilo…………..Na kumbuka, baada ya ile ishara ilipo dhihirishwa kikamilifu kwa Ibrahimu na kundi lake, jambo ambalo lilifuatia ilikuwa ni kubadilishwa. Sasa tumekwisha kuona kila kitu kupitia kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, kufanywa wana na ishara na maajabu yake, kuwa katika uwepo wake kupambanua mawazo ya moyo na kadhalika, kama alivyosema “kama ilivyokuwa siku za sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja wake mwana wa Adamu” (Luka 17:30). Tunaona yale yaliyotokea sasa. Kitu gani kilifuatia? Badiliko la mwili. Sasa, inavyoonyesha kuwa tunamtazamia mwana tulie mngojea. Utukufu. Hiyo ni kweli? Hatuwezi kumlaki yeye katika miili hii. Kama tukibadilishwa na kuwa vijana wanaume na wanawake, bado hatuwezi kukutana naye, kwa sababu inabidi tumlaki yeye hewani. Lazima kuwe na jambo fulani litendeke. Lazima tubadilishwe na kunyakuliwa kwa kanisa, na badiliko la miili ya watakatifu waliolala ili kukutana na Bwana Yesu Hewani.

Kanisa, kama umejitenga mwenyewe na Madhehebu na uchafu wote na mambo ya dunia, na mambo yote ambayo yana kushikilia katika kanuni na taratibu zilizotungwa na watu, na mambo kama hayo, umejitenga nayo mwenyewe, Angalia juu. Kuwa tayari. Moto utaenda kushuka siku moja ya siku hizi. Mungu atamuachia Yeye aje, katika uzuri wa kupendeza. Je wewe utakuwa tayari wakati ajapo? Utakuwa tayari kwenda naye wakati ajapo? Kule kunyakuliwa kwa siri kwa Bibi arusi wa kimbinguni…………Ataumbika kutoka hali ya kufa kwenda hali isiyopatikana na kufa; kubadilishwa mara moja, katika kufumba na kufumbua. Sisi tulio hai tutakaosali hatutawatangulia wao waliolala mauti.

Tunaingia katika wakati mwingine; tunaingia katika wakati wa kunyakuliwa. Unajua, kanisa haliwezi kwenda katika hali lilillo nayo, na haliwezi kamwe kuwa zuri; lazima lizidi kuharibikiwa (2 Wathesalonike 2:1-3). Wangapi wanajua hilo waseme, “amina”. Lazima lizidi kuharibikiwa na haliwezi kwenda hivyo lilivyo, unaona, lazima kuwepo kitu fulani na kinaendelea sasa

hivi marafiki. Kipo sasa. Safari inaendelea kwa Bibi arusi. Hiyo ni kweli na hiyo ni HII ASEMA BWANA.

Tunasubiri ule utimilifu wa kufanywa wana (Rum 8:23). Huu utafanyika lini? Katika ufufuko wa kwanza. Hapo ndipo miili yetu itabadilishwa kutoka kwenye hii miili miovu tulionayo na kuwa na mwili kama mwili wake mwenyewe wa utukufu, kwa maana tutamuona Yeye kama alivyo, nasi tutakuwa kama Yeye (1Yohana 3:2-3) Yesu alisema, "ukiuambia mlima huu………" (Marko 11:23). Na mmesikia yale yanayotendeka; hiyo ndio huduma tunayoingia sasa, tuko kileleni mwa barabara, karibu Bwana Yesu atakuja na tunapaswa kuwa na Imani ya kunyakuliwa katika kanisa, ambayo inaweza kutufanya tubadilishwe mara moja kwa kufumba na kufumbua ili kwenda, au hatutaweza kwenda. Lakini usitie shaka, itakuwa pale itakuwa pale. Na nguvu ya kanisa hili itakapoinuka, itawaleta wapendwa wao, nguvu ya kanisa lile itawaleta wapendwa wengine; hapo sasa kutakuwepo na ufufuo wa jumla. Tunalitazamia hilo.

Uwepo wake mkuu wa utukufu utaikumba dunia.

"Anakuja katika mawingu" (ufunuo 1:7). Oh, Nalipenda hilo. "Mawingu" kutakuwepo na wimbi baada ya wimbi la utukufu wake utakaopita duniani, na ufufuo wa watakatifu utafanyika. Wakati Roho Mtakatifu aliyebarikiwa ambaye aliishi ndani ya mioyo yao, na walipokufa maiti zao zililala pale, na alama za machozi katika videvu vyao na mambo kama hayo, wakawekwa nje pale makaburini kule. Wimbi kuu la Roho yuleyule, na wimbi baada ya wimbi la "Whoossh".

Yeye aliyekuwa wa mwisho atakuwa wa Kwanza, na yeye aliye wa kwanza atakuwa wa mwisho" (Mathayo 20:16). Itakuwaje hiyo? Huo ni utaratibu wa ufufuo. Sitamjua yoyote katika kizazi kabla yangu au kizazi baada yangu. Nitawajua wale wa kizazi hiki. Na kila kizazi kitakuja kwa mpangilio, hasa kama walivyokufa/walivyozikwa. "Wao walikuwa wa mwisho watakuwa wa kwanza" Hakika, lazima iwe hivyo. Unaona nitawajua watu wangu. Mtu aliyefuatia, baba yangu, atawajua watu wake; babu yake watu wake, na kuendelea hivyo mpaka chini.

Wimbi baada ya wimbi, baada ya wimbi, na watakatifu wakiinuka kutoka kila mahali, je si itakuwa ni la kupendeza/ ajabu sana. Amina.

Swali lingine: je Bibi Arusi atakusanywa mahali pamoja wakati wa unyakuo………Ndiyo, Bibi arusi atakusanywa mahali pamoja. Hiyo ni kweli, lakini hilo ni baada ya ufufuo. Kwa maana sisi tutakaosalia hata wakati wa



kuja kwa Bwana hakika hatuta watangulia (au kuwazuia) wale walio lala mauti (dunia nzima); kwa maana tarumbeta ya Mungu Italia, nao waliokufa katika Kristo watafufuka nasi tutanyakuliwa pamoja nao kumlaki Bwana hewani" kwa hiyo Bibi arusi watakuwa wote pamoja wanapoenda kumlaki Bwana. Watakuwa pamoja, lakini siyo lazima imaanishe watakuwa wamekaa mahali pamoja, kama hivi; kwa sababu Bibi arusi aliyelala mauti yuko katika sehemu zote za dunia, kutoka pembe ya dunia (Arctic) mpaka sehemu za joto na mashariki mpaka magharibi, kutoka kaskazini mpaka kusini.

Yesu alisema, "mwana wa Adamu atakapoonekana" (Matayo 24:27-31) kwanini, alisema, itakuwa kama nuru inayoangaza kutoka mashariki hata mpaka magharibi" sehemu yote, utakuwepo ufufuko, unyakuo, na hao tutakwenda. Na kabla ya kwenda juu kumlaki Yeye………………………..

Sasa, jambo la kwanza linalotokea baada ya kufufuka ……….wale ambao wanaishi watabakia tu hivyo…………..ufufuko utaanza kufanyika, ufufuko wa wale waliolala. Kutakuwa na wakati wa uamsho, na wale ambao wamelala katika mavumbi sasa, siyo wale waliolala katika dhambi, kwasababu wataendelea kulala. Hawaamshwi mpaka miaka elfu ipite. Lakini wale walio lala mauti wataamshwa kwanza, na miili hii ya mauti itavaa kutoharibika katika neema ya unyakuo wa Bwana. Na hapo tutakusanyika pamoja, sasa sisi tulio hai ambao tumebakia, tutabadilishwa, miili hii inayokufa haitaonja mauti, lakini kwa mara moja, kutakuwa na uvumi kama upepo juu yetu, na utakuwa umebadilishwa. Unabadilishwa kama Ibrahimu alivyobadilishwa, kutoka mtu mzee kuwa kijana mwanamke. Ni nini hili badiliko la mara moja? Na baada ya muda mfupi unatembea kama wazo, na unaweza kuwaona sasa wale waliofufushwa tayari. Oh saa ya ajabu. Halafu tutakusanyika nao na kunyakuliwa pamoja nao kumlaki Bwana hewani.

Siyo, lazima, kama mjomba wako amezikwa India na kwamba lazima aletwe kentuki mashariki. Haijalishi yuko wapi…………..wale walio kufa baharini watafufuka kutoka baharini. Wale waliouawa kwenye viwanja vya michezo na kuliwa na simba, wale waliotupwa kwenye matanuri ya moto na hata mfupa wao hautaachwa au mavumbi, watainuka kama walikuwa Roma au viwanja vya michezo vya Roma au pengine walikuwa kwenye misitu ya kusini ya nchi za joto, au sehemu za kaskazini za barafu, watainuka kutoka katika wafu na kubadilishwa; na kuletwa juu; na walio hai watabadilishwa kwa mara moja, kufumba na kufumbua jicho na kunyakuliwa pamoja.

Angalia wale wamisionari waliokufa katika mashamba ya Afrika. Angalia wale waliokufa ng'ambo kule kwenye nchi za barafu za kaskazini. Angalia wale waliokufa katika viwanja vya michezo, sehemu zote za dunia, katika

Kongo, na sehemu zote kuzunguka dunia. Wamekufa kila mahali katika china, Japani, kuzunguka dunia; na kuja kwa Bwana kutakuwa ni jambo la dunia yote, ule unyakuo.
Tazama lile badiliko. Watakuwepo wawili kitandani; mmoja atwaliwa na mmoja aachwa, 'wakati huohuo watakuwepo wawili shambani; mmoja atwaliwa na mmoja aachwa, "mmoja katika upande wa giza la dunia na mmoja katika upande wa dunia wenye nuru (Luka 17:34-36). Itakuwa ni unyakuo wa dunia yote. Ndio kanisa lote litakuwa pamoja, lakini ni baada, baada ya ufufuo na unyakuo kuanza.

Unasema Roho Mtakatifu ni muhuri? Waefeso 4:30 ilisema, "msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu ambaye kwa huyo mmetiwa muhuri hata siku ile ya ukombozi" Hiyo ni muhuri ya pasaka halisi. Kuonyesha dhambi zimekwisha kulipwa, kwa ajili yako, na Mungu amekukubali, na umetiwa muhuri ndani ya Kristo kwa Roho Mtakatifu. Dhambi imekwisha. Muhuri wa milele umekwisha malizika/kamilika.

Sasa, tumefufushwa leo. Kwa nini tunaweza kuwa na muda kama huo juu ya mambo ya Mungu? Kwa sababu tumefufushwa. "wale aliowajua kimbele, aliwaita; wale aliowaita, Aliwahesabia haki; wale Aliowahesabia haki, aliwatukuza (Rumi 8:30). Sasa hivi tumefufushwa. Tumefufushwa kutoka ndani, sio kwa nje. Oh unaona, sio kutiwa Muhuri kwa namna hii nje, lakini kutiwa Muhuri ndani. Sasa hivi tumefufushwa. Unajuaje? Biblia ilisema hivyo. Amen. Sasa hivi tumefufushwa pamoja naye katika ufufuo wa kiroho. Hili Neno "kuhuishwa" linamaanisha nini? "Kuhuishwa" kunamaanisha "kufufushwa". Hiyo ni kweli. Tayari sisi tumefufushwa sasa hivi, tukiwa tumekaa pamoja katika ulimwengu wa Roho ndani ya Kristo Yesu (Waefeso 2:6) Tukoje/kwa Roho mmoja tumebatizwa ndani ya mwili na kutiwa muhuri milele.

Sasa hivi tumefufushwa kiroho. Tumefufushwa kutoka kwenye nini? Kutoka kwenye maisha ya dhambi; wakati mmoja tulikuwa wenye dhambi na tulipenda mambo ya dunia
Sasa, hivyo ndivyo Mungu anavyofanya kwa kanisa lake. Anawachonga watu, na kuliweka kwa namna ambayo ni kamilifu, kwamba kile kifuniko, Kristo, anapokuja, kinalingana kabisa na jengo lote pamoja, na baadaye ufufuko wa wote, kanisa linaenda juu. Kile kifuniko ……………………

Kamwe usimuache shetani akuambie kitu kingine chochote. Tukiwa sehemu ya mtu mmoja kwa mwingine, tu sehemu yake, na tu wenyeji katika ufalme wake, tukifurahia pamoja baraka za ufufuo.



Uko tayari umefufuka. Mungu alipo mfufusha, Alikufufusha wewe; mwana yuko juu yako sasa (Warumi 6:4-6). Na sasa unakuwa katika kuchanua kwa maisha kama vile alivyokuwa amefufuka kikamilifu katika siku ya mwisho. Kile unachopaswa kuwa unacho sasa. Unajuaje? Nafsi yako imebadilika, si ndiyo? Mwili wako umekuwa mtiifu kwa hiyo, si ndiyo? Katika utiifu kwa kitu gani? Kanisa? Neno ambalo ni uzima. Halafu sasa umefufushwa kutoka katika wafu.

Sisi sote tumefufushwa pamoja na tutafufushwa katika siku ya mwisho hata kama roho zetu ziiache miili yetu, hata kama miili yetu iwe na kutu, ingeenda kwenye mavumbi, hata kama ingeunguzwa, hata iwe chini ya bahari – Biblia ilisema.

- Malaika alijimwaga mwenyewe juu ya bahari na kila kitu kilichokufa kilifufuka.

Hakuna kitu kiwezacho kutuficha au kututenga sisi kutoka kwa Mungu yule tumpendaye sana, ambaye ametufufusha sisi pamoja (Rum 8:35-39) Sasa, angalia, wakati nguvu hii kuu ya Mungu inakuja kwa mwana wa Mungu, inamhuisha yeye; Roho wa uzima anaingia ndani yake. Halafu inakufanya nini? Inawakalisha wao katika ulimwengu wa Roho, sasa hivi, siyo watakuwa, wako hivyo sasa.

Sasa hivi tumesha fufushwa tayari; ile nguvu ya kuendesha na vitu imeenda kufanya kazi kutuhuisha sisi, na tumehuishwa katika uwepo wa Mungu, ambapo Roho wake yuko. Na sasa tumeketi pamoja katika ulimwengu wa Roho ndani ya Kristo Yesu; ndani ya Kristo Yesu, tukikaa hapo, tukiwa tumefufushwa kutoka kwa wafu tu sehemu ya hiyo. Kama u sehemu ya Bibi Arusi, wewe ni wake, kwa sababu Bibi Arusi ni sehemu ya Bwana Arusi, unajua (Waefeso 5:30-32).

Kwa hiyo tunaona kuwa ni jambo lilelile, a atafanya hasa kile alichoambiwa yeye (Bibi Arusi) kuwa Atakifanya katika siku hizi. Yeye (Bibi Arusi) hatakuwa mlaodikia, hata kwa hali yoyote, Vuguvugu. Lakini atakuwa katika moto na Mungu atakuwa anatembea katika Roho wa Mungu.

Lazima awepo muumba kama kuna viumbe (Wakolosai 1:15-17) Na kama kuna viumbe, vimeumbwa na Muumbaji. Na kazi ya mtu yeyote inamueleleza yeye mwenyewe. Kama ni seremala mzuri, anafanya kazi nzuri, anajenga. Na kama ni fundi mzuri wa umakanika vyuma viendeshavyo, unafanya kazi nzuri. Kazi yako inakueleleza wewe. Na uumbaji wa Mungu unamueleleza Mungu. Na Mungu alifanya kila kitu kwa kusudi. Na kila kitu kinachotumika kwa kusudi la Mungu, kinapokufa kina ufufuo. Niambie kitu kimoja.

Na kama mtu akitumika katika kusudi la Mungu, kutakuwa na ufufuo kwa hakika kama iwezavyo kuwa. Kitu pekee unachopaswa kufanya, ni Mungu anasubiri tu Muda, kama vile tu Afanyavyo sasa. Wale wapagani ambao kamwe hawajasikia injili watafufuliwa katika wakati huo (Kristo na Bibi Arusi wanaporudi kwa utawala wa miaka Elfu), na wana wa Mungu watadhihirishwa. Kama watatawala, lazima awe na kitu fulani cha kutawala juu yake; mamlaka yake (Himaya) "nao wakatawala pamoja na Kristo" na Kristo akatawala Mataifa kwa fimbo ya chuma. (Ufunuo 2:26-28; Zaburi 2). Halafu wana wa Mungu wakiwa na mamlaka kama yale aliokuwa nayo Alipokuwa hapa. Utakuja utawala wa miaka Elfu (Ufunuo 20:4-6).

**Nukuu za kingereza**

"kuchomoza kwa jua" uk. 29,50; "kutoa presha (msukumo)" (62-0518), Aya 112p. "jehova atajipatia "(sehemu 1 62-0705), Aya 12. "kwenda nje ya kambi. "Aya 22. Mungu katika urahisi" uk 58
"Maswali na majibu" (59 – 1223), swali no:105. "Israeli pale katika bahari nyekundu". Aya 76-80. "kumkumbuka Bwana" Aya 35-44
"Muhuri ya kweli ya pasaka" (61-0402(, Aya 138-143, 124-
134
"Muungano usioonekana wa Bibi Arusi" uk 46 + 55 ":ufunuo sura ya tano sehemu 1, "Nyoka aliyejeruhiwa" Aya 108. Maswali na majibu juu ya Roho Mtakatifu", C.O.D. uk 420 "Nyakati saba za kanisa" 54-0512, Aya 97, "Maswali na majibu "(64-0823m) swali no: 240, COD uk 933. "Mahali alipopachagua Bwana pakuabudia" (65-0425), Aya 137, "Maswali na majibu" 62-0527, COD uk 723.

---

*Jiwe la kujengea la kiroho No: 134 kutoka kwenye Neno lililo funuliwa la saa hii, yamekusanywa na Gerd Rodewald, Friedenstr. 69, D – 75328 sechomberg, Germany. Simu (+49) 72357613, Fax: (+49) 72353306.*

---

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao utakuwa ni Biblia moja kwa moja na kazi ya haraka itaizunguka dunia, mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu ya Mungu iliyokusudiwa kimbele imesikia.*

*Ndugu Branham katika mwenendo na utaratibu wa mafundisho uk. 724.*

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili andika kwa :*
*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*